JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

(OR-TAMISEMI)

WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA (TARURA)

Na

WAKALA WA BARABARA TANZANIA (TANROADS)

PROGRAMU YA MAENDELEO YA BARABARA KWA USHIRIKISHAJI WA JAMII NA UFUNGUAJI WA FURSA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI (RISE)

(P164920)

RASIMU YA MWONGOZO WA MPANGO WA MAKUNDI YALIYO KATIKA HALI HATARISHI (VGPF)

DISEMBA 2020

MUHTASARI WA KIUTENDAJI

E1. Serikali ya Tanzania kupitia kwa mawakala wake wa kiutendaji, yaani Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaandaa Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi. Programu hii inahusisha jitihada za kuboresha upatikanaji wa barabara vijijini na kutoa fursa za ajira kwa wananchi katika maeneo ya vijijini yaliyochaguliwa na kujenga uwezo katika usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kujumuisha mbinu za ushirikishwaji wa jamii Mwelekeo wa sasa ni kuhakikisha sekta ya usafirishaji wa watu na mizigo kuelekea na katika maeneo ya vijijini yenye fursa za kilimo ambazo bado hazijaguswa inakuwa salama na yenye ufanisi. Programu hii itasaidia pia kuyafikia maeneo mengi nchini Tanzania ili kuyafanyia maboresho mahususi na ukarabati wa mara kwa mara katika barabara za mikoa na wilaya. Programu ina vipengele vinne ambavyo ni:

- Kipengele cha 1: Ujenzi na Ukarabati wa Barabara Vijijini
- Kipengele cha 2: Uimarishaji wa Taasisi na Rasilimali Watu Kipengele cha 3: Uhusishwaji; Ushirikishwaji na Usalama wa Jamii
- Kipengele cha 4: Ushughulikiaji Matukio ya Dharura

Mwongozo wa Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGPF) unatekelezwa kwa kusaidiana na miongozo ifuatavyo:

- Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESMF)
- Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP)
- Mpango wa Uwajibikaji katika Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESCP)
- Mpango wa Ufuatiliaji wa Masuala ya Kijinsia (GAP)

E2. TARURA na TANROADS wameandaa Mwongozo wa Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGPF) kwa ajili ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi. Lengo la Mwongozo huu ni kutoa maelekezo kuhusu namna ya kuandaa Mipango ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGPs) kwa ajili ya miradi-midogo iliyomo ndani ya Programu hii. Hata hivyo, Mwongozo huu ni kitendeakazi kinachosaidia kuhakikisha kwamba usanifu na utekelezaji wa miradi-midogo iliyomo ndani ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi unafanywa kwa kuzingatia ubora wa hali ya juu, haki za binadamu, uchumi na utamaduni wa makundi maalum. Pia, lengo lingine ni kuboresha unufaikaji wa makundi yaliyo katika hali hatarishi katika maeneo ambayo utekelezaji wa miradi-midogo ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi unatekelezwa. Mwongozo kwa ajili ya Uwezeshaji wa Makundi Maalumu (VGPF) unatoa maelezo ya kina kuhusu kanuni, Sera, Miongozo na Taratibu zilizokubaliwa ambazo zitahusishwa katika utekelezaji wa miradi midogo ya Programu hii. Pia, utasaidia kufikia matokeo ambayo yanaafikiana na Sheria za Kitaifa kuhusiana na Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi na Mwongozo wa Benki ya Dunia wa Mazingira na Masuala ya Kijamii. Makundi Maalumu yanayorejelewa katika VGPF yana sifa zifuatazo kama zilivyofafanuliwa katika Kiwango Nambari 7 cha Kimazingira na Kijamii (ESS7):

- Kujitambua kuwa ni wahusika wa kundi fulani la kijamii na kitamaduni na utambulisho huo ufahamike kwa watu wengine;
- Kuwaleta pamoja watu wanaoishi katika maeneo tofauti ya kijiografia, maeneo ya kiukoo au maeneo yanayotumiwa au yenye kazi za msimu, pamoja na maliasili zilizopo katika maeneo hayo;
- Taasisi za kitamaduni, kiuchumi, kijamii au kisiasa ambazo ni tofauti au zimejitenga kutoka katika jamii au tamaduni kubwa; na
- Lugha au lahaja ambayo ni tofauti na lugha rasmi inayotumiwa katika nchi au kanda husika.

E3. Majukumu katika Utekelezaji wa Muongozo wa Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGPF): TARURA na TANROADS watawajibika katika kupanga na kusimamia mipango yote ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGs). Katika ngazi ya Mikoa, TARURA (katika Mikoa yote inayoshiriki kwenye miradi) na TANROADS (Ndani ya Mkoa wa Iringa) itamteua Mtaalamu mmoja (1) wa Ustawi wa Jamii ambaye atawajibika katika maendeleo ya jamii na udhibiti wa vihatarishi ikiwa ni pamoja na mchujo wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi katika miradi-midogo na uandaaji wa Mipango ya Makundi hayo sambamba na Muongozo wa Mpango wa Makundi Maalumu (VGPF). Mwajiriwa wa ngazi ya Mkoa atafanya kazi chini ya usimamizi na mwongozo wa Timu ya Masuala ya Kumazingira na Kijamii kutoka Makao Makuu ya Dodoma (TARURA) na Dar es Salaam (TANROADS), mtawalia.

E4. Miongozo ya Sera inayosaidia Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi: Inatambulika kwamba Serikali ya Tanzania haina Sera mahususi au Sheria inayohusu Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi. Hata hivyo, pamoja na kuunga mkono Azimio la Umoja wa Mataifa la mwaka 2007 juu ya haki za raia wazawa, bado haijaandaa Sera yoyote au Sheria mahususi inayoyahusu makundi ya aina hiyo. Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi hautawanufaisha tu katika utofautishaji wa Sera na Sheria za kitaifa ambazo zinaakisi maslahi ya raia wazawa kama ilivyoelezwa hapo chini lakini pia yale yanayotolewa kwenye Kiwango Nambari 7 cha Kimazinira na Kijamii (ESS7). Mwongozo wa Mpango wa Uwezeshaji Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGPF) umeandaliwa kwa kufuata Sera na Kanuni zifuatazo za Kitaifa pamoja na Sera za Kimataifa zinazohusu utendaji bora:

- Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995;
- Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000;
- Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997;
- Sera ya Taifa ya Jinsia ya Mwaka 2002;
- Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Novemba 20, 2009;
- Sera ya Taifa ya VVU/UKIMWI ya Mwaka 2001;
- Sheria ya Ardhi Na. 4 na 5 ya Mwaka 1999;
- Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012;
- Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997;
- Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Sehemu ya 7(1);
- Sera ya Urithi wa Utamaduni ya Mwaka 2008;
- Mwongozo wa Benki ya Dunia wa Mazingira na Masuala Kijamii.

E5. Maandalizi ya Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yatafanyika kama inavyofafanuliwa katika Mpango wa Uwezeshaji Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi ulimo ndani ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi kama ifuatavyo:

- Mchujo wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yaliyopo;
- Kufanya tathmini ya kijamii;
- Kubainisha matokeo na kuazimia hatua za kulishughulikia suala hilo;
- Maandalizi ya Mpango wa Kuyawezesha Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi;
- Kujenga Uwezo;
- Maamuzi ya Benki kuhusu Uwekezaji wa Mradi.

Mipango ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi katika miradi-midogo itaandaliwa huku ikiakisi shughuli za kijamii na kitamaduni, jiografia ya maeneo na shughuli za kimaisha za jamii husika pamoja na matokeo na vihatarishi vya mradi katika Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi. Vipengele mahususi vya mradi-mdogo katika Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi ni: matarajio, mahitaji, na machaguo yanayopendelewa kwa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yaliyoathirika; taasisi za kijamii katika serikali za mitaa, imani, mipaka ya kiukoo, na ruwaza za matumizi ya rasilimali miongoni mwa makundi maalumu yaliyoathirika ambayo yanahusiana na mradi; matokeo chanya na hasi pamoja na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza kwenye makundi maalumu; hatua za kuchukua ili kuzuia au kupunguza vihatarishi na athari mbaya; matakwa ya Idhini Huru ya Ufahamisho wa Awali (FPIC), kama yatahitajika; hatua za kuchukua ili kuhakikisha kwamba faida za mradi zinaongezeka kwa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi; uwezekano wa kuyahusisha Asasi za Kijamii (CBOs) na Asasi Zisizo za Kiserikali (NGOs) kuwakilisha Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGs); mahitaji maalumu yanayohusiana na uhusishaji wadau na Mkakati wa Ushuhgulikiaji Malalamiko (GRM) katika Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (VGs); upangaji wa bajeti; na ufuatiliaji.

Mipango yote ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi (PSVGPs) itakayoandaliwa ndani ya miradi itahusisha maudhui yafuatayo, kama yanavyohitajika:

- Muhutasari wa mwongozo wa kisheria na kitaasisi unaoweza kutumika katika Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi.
- Taarifa za msingi kuhusu sifa za kidemografia, kijamii, kiutamaduni, na kisiasa kwa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yaliyoathirika katika jamii, ardhi na maeneo ambayo kwa asili yanamilikiwa au yanatumiwa kimazoea, au yametengwa, na maliasili wanazozitegemea ambazo zinahusiana na mradi.
- Muhutasari wa tathmini ya kijamii.
- Muhtasari wa matokeo ya ushauri wa wadau kuhusu athari za Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi zilizobainishwa wakati wa maandalizi ya mradi.
- Mwongozo wa kuhakikisha idhini huru ya ufahamisho wa awali kwa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yaliyoathirika wakati wa utekelezaji wa mradi mdogo na uthibitisho wowote mara utakapopatikana.
- Mpangokazi wa hatua zitakazochukuliwa kuhakikisha kwamba Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yanapata maslahi ya kijamii na kiuchumi yaliyo mwafaka kiutamaduni, pamoja na, kama itafaa, hatua za kuboresha uwezo wa mawakala katika utekelezaji wa miradi.
- Ikiwa athari mbaya zinazoweza kujitokeza katika Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi zimebainishwa, mpangokazi mwafaka wa kuziepuka, kuzipunguza makali, kuzipunguza

kabisa au kufidia athari hizo mbaya kutegemeana na taarifa zilizowasilishwa kutokana na tathmini ya jamii.

- Makadirio ya gharama na mpango wa fedha kwa ajili ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi; kila mradi utachungua gharama zote za kusaidia na kuyarudisha Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi katika hali ya kawaida.
- Taratibu zinazofahamika na mwafaka kwa mradi za kushughulikia malalamiko ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yaliyoathirika ambayo yameibuka kutokana na uwekezaji wa mradi. Wakati wa kuandaa taratibu za malalamiko, Serikali inazingatia upatikanaji wa msaada wa kimahakama na mbinu za kukabiliana na migogoro iliyozoeleka miongoni mwa Makundi hayo.
- Mbinu na viashiria mwafaka vya mradi kwa ajili ya kufuatilia, kutathmini, na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kuyawezesha Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi. Mbinu za ufuatiliaji na tathmini lazima zihusishe mipangilio ya idhini huru ya ufahamisho wa awali kwa makundi yaliyoathirika.

E6. Ushiriki wa Wadau wakati wa Usanifu na Utekelezaji Mradi: Ushiriki wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi katika vipengele vya uteuzi, usanifu na utekelezaji wa mradi, kwa kiasi kikubwa utategemeana na mafanikio ya malengo ya Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi. Kuhakikisha kwamba faida za mradi zinadhihirishwa na athari mbaya zinazoweza kuwapo zinawekwa bayana, Timu ya TARURA na TANROADS itashughulikia mapema utoaji ushauri kwa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yanayoweza kuathirika pamoja na wale wanaofanya kazi pamoja na makundi hayo au wenye uelewa kuhusu masuala na mahitaji yanayohusu maendeleo ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi. Malengo makuu yatakuwa kuchunguza masuala yafuatayo:

- Kutafuta maoni/mrejesho wao juu ya uongezaji wa faida, upatikanaji na jinsi ya kuzuia au kupunguza uwezekano wa athari mbaya zinazohusishwa na mradi;
- Kubainisha hatua za kuchukua ili kupunguza athari ambazo ni rafiki kiutamaduni; na
- Kutathmini na kutumia fursa za elimu, ambazo zinaweza kuhamasishwa na Tathmini ya Kijamii ambazo zitakamilisha hatua zinazotakiwa ili kupunguza athari mbaya.

Mkakati wa mawasiliano katika Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi ni:

- Kuwezesha ushiriki wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi katika masuala na mahitaji ya maendeleo ya makundi hayo kwa kuzingatia jinsia na uwakilishi wa umri; Vijana; Taasisi za Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi yaliyozoeleka, wazee katika jamii; na Asasi za Kijamii (CSOs), Asasi za Kiraia (CBOs) na Asasi za Kiimani/kidini (FBOs).
- Kuwapatia taarifa muhimu kuhusu vipengele vya mradi, ikiwa ni pamoja na athari mbaya zinazoweza kujitokeza, kuandaa na kutoa ushauri katika namna inayowahakikishia uhuru wa kueleza mawazo na vipaumbele vyao.
- Kuyaandika na kuyatunza masuala yote yanayojitokeza katika mkutano wa mashauriano, na mtazamo wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi kuhusu mradi unaopendekezwa pamoja na athari zinazohusiana na Mpango huu, hususani athari mbaya, na maoni/mrejesho uliotolewa na Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi; na wajibu wa jamii kusaidia au maridhiano ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi.

E7. Ushauri kuhusu Mwongozo wa Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi: Wakati wa maandalizi ya Mwongozo huu wa Uwezeshaji wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi katika Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi, kulitolewa ushauri kutoka katika idara zinazohusika za Serikali tarehe 09 Januari, 2020. Ushauri mwingine ulitolewa na kutoka katika Asasi zisizo za Kiserikali na Asasi za Kijamii zilizowakilisha matakwa ya Makundi Maalumu katika ngazi ya Taifa kwenye warsha iliyofanyika Dodoma tarehe 21 Januari, 2020. Ushauri wa nyongeza ulitolewa na Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali kati ya tarehe 07 na 11 Februari, 2020. Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi ambayo yataathiriwa na miradi midogo yataombwa ushauri wakati wa maandalizi ya Miongozo ya Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi.

E8. Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko: Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko katika Mwongozo wa Mpango wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi utafuata ule wa Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi ulioelezwa katika Mpango wa Ushirikishaji Wadau. Kwa miradi midogo iliyo chini ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi, kunapaswa kuandaliwa Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko ambao unatambua maarifa, mienendo na kaida za jamii ambapo TARURA/TANROADS kupitia mashauriano na Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi watasaidia kutambua na kukubaliana na makundi hayo katika:

- Kuwapo kwa mikakati ya usuluhishaji migogoro ndani ya jamii;
- Taratibu, utendaji, pamoja na jinsi mchakato wa kushughulikia usuluhishaji wa migogoro ulivyo katika jamii za Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi;
- Wasemaji wakuu wa usimamizi wa migogoro katika jamii za Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi;
- Mchakato wa uhusishaji mkakati wa wenyeji unaotumiwa kusuluhisha migogoro ili kuendana na utekelezaji wa mradi huku mila za wenyeji na michakato ya usuluhishaji migogoro zikizingatiwa;
- Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko kwa kufuata michakato iliyoelezwa hapo juu na kuijaamisha kwa viongozi wa jamii za Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi, watu walioko katika wa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi, uongozi wa Kijiji, na wadau wengine katika maeneo ya miradi midogo.

Maelezo mahususi ya malalamiko yanayohusiana na Unyanyasaji na Ukatili wa Kingono (SEA) yanayoweza kusababishwa na mradi yatajumuishwa ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka na kuna usiri kwa walionusurika. Ili kushughulikia vizuri vihatarishi vya Ukatili wa Kijinsia, Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko unapaswa kukamilika kabla ya wakandarasi hawajaanza kupeleka mitambo katika sehemu ya kazi.

E.9. Ufuatiliaji na Tathmini

- Utekelezaji wa Mwongozo wa Mpango wa Makundi Yaliyo Katika Hali Hatarishi (VGPF) na Mipango ya Makundi Yaliyo Katika Hali Hatarishi (VGPs) utasimamiwa na kufuatiliwa na Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU); na matokeo yatarekodiwa katika taarifa za maendeleo ya miradi ambazo zitawasilishwa Benki ya Dunia;

- Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) kitahakiki ukusanyaji wa taarifa za awali kuhusu Makundi Yaliyo Katika Hali Hatarishi (VGs); na
- Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) kitamuhusisha Mtaalamu Mshauri wa nje ya mawakala wa utekelezaji, ili kufanya kazi ya ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa Mipango ya Makundi Yaliyo Katika Hali Hatarishi (VGPs).